SHERIA YA FEDHA YA SERIKALI ZA MITAA
(SURA YA 290)

_____

SHERIA NDOGO

Zimetungwa chini ya kifungu cha 7(1) na 16(1)

SHERIA NDOGO ZA (ADA NA USHURU) ZA HALMASHAURI YA WILAYA YA NSIMBO ZA MWAKA 2017

SEHEMU YA KWANZA
UTANGULIZI

Jina na tarehe ya kuanza kutumika

1. Sheria Ndogo hizi zitajulikana kama Sheria Ndogo za (Ada na ushuru) za Halmashauri ya Wilaya ya Nsimbo za mwaka 2017 na zitaanza kutumia baada ya kutangazwa kwenye Gazeti la Serikali.

Matumizi

2. Sheria Ndogo hizi zitatumika katika eneo lote lililo chini ya mamlaka ya Halmashauri ya Wilaya ya Nsimbo.

Tafsiri

3. Katika sharia ndogo hizi isipokua pale itakapoelezwa vinginevyo:-
"Ada na ushuru" maana yake ni malipo yanayolipwa kwa Halmashauri au wakala wake kwa ajili ya huduma, vibali, au leseni mbalimbali zitolewazo na Halmashauri.
"Afisa Mwidhiniwa" maana yake ni Afisa yeyote wa Halmashauri atakayeteuliwa kusimamia utekelezaji wa Sheria Ndogo hizi;
"Chombo cha Usafiri" maana yake ni chombo chochote kinachotumika kusafirisha mtu, watu au mizigo kutoka sehemu moja kwenda nyingine isipokuwa mkokoteni, au wanyama wanaotumika kama kusafirisha watu au mizigo.
: Halmashaurti " maana yake ni Halmashauri ya Wilaya ya Nsimbo;
"Kituo cha Mabasi" maana yake ni eneo maalum lililotengwa na Halmashauri kwa madhumuni ya kupakia na kutelemsha abiria na mizigo ya abiria;

" Machinjio" maana yake nis ehemu iliyotengwa na Halmashauri kwa ajili ya kuchinjia wanyama na kuanika ngozi;
" Madini ya Ujenzi" maana yake ni kokoto, mawe, changarawe, mchanga, marumaru, kifusi, udongo mfinyanzi, au chochote kinachochimbwa na kupatikana katika mamlaka ya Halmashauri kwa shughuli za ujenzi.
"Maegesho" maana yake sehemu yeyote iliyotengwa na Halmashauri kwa jili ya kuegesha chombo cha usafiri kwa muda.
" Masoko" maana yake ni sehemu yoyote iliyotengwa na Halmashauri kwa ajili ya kuuza na kununua bidhaa;

"Mnada" maana yake ni sehemu iliyotengwa na Halmashauri kwa ajili ya kuendesha shughuli za kuuza na kununua bidshaa;
"Mkurugenzi"maana yake ni Mkurugenzi Mtendaji Halmashauri ya Wilaya ya Nsimboau Afisa yeyote wa umma atakayeteuliwa kutekeleza majukumu ya mkurugenzi.
"Usajili wa Vyombo vya usafiri" maana yake ni utaratibu utakaowekwa na Halmashauri wa kuorodhesha idadi ya vyombo vya usafiri vinavyofanya biashara ndani ya mamlaka ya Halmashauri:
"Ushuru wa madini ya ujenzi" maana yake ni ushuru utakaotozwa kwa kibali cha uchimbaji wa kokoto, mawe, udongo mfinyanzi, au chochote kinachochimbwa na kupatikana katika mamlaka ya Halmashauri kwa shughuli za ujenzi;
" Wakala" maana yake ni mtu, Taasisi, kampuni, au asasi yeyote iliyoteuliwa kisheria na Halmashauri kukusanya mapato kwa niaba ya halmashauri.

SEHEMU YA PILI
NAMNA YA KUKUSANYA ADA NA USHURU

Ada na Ushuru

3.-(1) Halmashauri itatoza Ada na Ushuru mbalimbali kwa ajili ya vibali, leseni na huduma zitolewazo katika eneo la mamlaka ya Halmashauri kwa mujibu wa viwango vilivyowekwa katika jedwali la kwanza la sharia ndogo hizi.
(2) Ada na Ushuru utozwayo chini ya sharia Ndogo hizi utalipwa kabla ya huduma kutolewa.
(3) Huduma zitakazotozwa Ada na ushuru katika Sheria Ndogo hizi ni:-
(i) Kibali na ushuru wa madini ya ujenzi;
(ii) Ada na kibali cha Matangazo ya biashara
(iii) Ada ya kukodi mali za Halmashauri;
(iv) Ada na vibali vya kuendesha shughuli za utamaduni na michezo.
(v) Ada ya huduma za machinjio, ukaguzi wa nyama na ushuru wa bucha
(vi) Ushuru wa Gulio na soko.
(vii) Ushuru wa mifugo na bidhaa za minada
(viii) Ada ya upimaji wa Ardhi na vibali vya ujenzi;
(ix) Ushuru wa stendi ya maegesho ya magari;
(x) Ada ya kuchangia uzoaji taka Mijini (emerging towns)
(xi) Ushuru wa mazao
(xii) Ada na ushuru wa huduma nyingine

Uwezo wa kubadilisha viwango vya ada na ushuru

4. Halmashauri itakuwa na uwezo wakubadilisha viwango vya Ada na ushuru pale itakpoona kuwa inafaa kwa kushirikisha wadau, na kutangaza katika sharia Ndogo hizi kama marekebisho.

Taratibu za kulipa Ada ya ushuru

5. (i) Itakuwa ni wajibu wa kila mtu anayetakiwa kulipa Ada na Ushuru kuhakikisha analipa Ada na ushuru kwa viwango vilivyoainishwa kwenye jedwali la sharia ndogo hizi.

(2) Muda wa kukusanya Ada na Ushuru utakuwa ni kuanzia sa kumi na mbili kamili (12:00) asubuhi mpaka saa kumi na mbili (12;00) jioni.

(3) Bila kuathiri masharti ya kifungu kidogo (2), Maafisa wa Halmashauri au Wakala anaweza kukusanya ushuru baada ya muda uliyotajwa hapo juu endapo atakuwa na kibali maalum kutoka kwa Mkurugenzi.

(4) Malipo ya Ada na Ushuru yatafanyiaka kila siku au kwa mwezi au kwa namna yeyote itakayokubalika kulingana na makubaliano yatakayowekwa kati ya Halmashauri/ Wakala na mlipa ada na ushuru.

(5) Malipo ya Ada na Ushuru ynayotozwa kwa Mujibu wa Sheria Ndogo hizi yatalipwa kwa Halmashauri au Wakala wake na kutolewa stakabadhi ya Halmashauri kama kielelzo cha malipo yaliyofanyika.

Uteuzi wa Wakala

(6) Halmashauri inaweza kumteua Kampuni, Asasi au Taasisi kukusanya Ada na Ushuru kwa niaba yake katika vyanzo vilivyoruhusiwa kutumia mawakala.

Wajibu Wakala

(7) Wakala aliyeteuliwa chini ya sharia Ndogo hizi atakuwa na wajibu wa:-

(a) Kukusanya na kupokea Ada na Ushuru katika eneo alilopangiwa kwa kiwango kilichoainishwa chini ya sharia Ndogo hizi:

(b) Kuwasilisha makusanyo yote kwa kuzingatia masharti ya Mkataba na Uwalaka;

© kuweka dhamana ya kusanyo la mwezi mmoja kabla ya kuanza makusanyo ambapo dhamana hiyo itarejeshwa mwisho wa mkataba.

Kumchukulia hatua za kisheria mtu yoyote ambaye atakiuka masharti ya sharia ndogo hizi;

SEHEMU YA III
MAKOSA NA ADHABU

Makosa

8(1) Itakuwa ni kosa kwa ;

A. Kwa wakala endapo;

(a) Kukusanya Ada na Ushuru bila kibali cha maandishi au mkataba toka kwa Halmashauri;

(b) Kujaribu au kukusanya ada na ushuru kwa kiwango tofauti na kilichotajwa na sharia ndogo hizi;

(c) Kushindwa kuwasilisha pungufu ya kiwango cha Ada na Ushuru alichokubaliwa katika mkataba: au kusanya Ada na ushuru kwa mbinu tofauti na alizoelekezwa na Halmashauri.

B. Kwa yeyote endapoi;

(a) Kushindwa kudharau, au kukaidi kukataa kulipa Ada na ushuru au kutekeleza agizo lolotealilopewa na Halmashauri kuhusiana na ulipaji wa Ada na Ushuru chini ya sharia Ndogo hizi;

(b) Atamshawishi mtu au kundi la watu kukataa au kukwepa kulipa Ada na Ushuru;

(c) Atatengeneza, atatyarisha, ataidhinisha utengenezaji, au atatunza nyaraka za uongo kwa nia ya kujipatia manufaa yatokanayo na ukusanyaji wa Ada na Ushuru mbalimbali ndani ya Halmashauri.

(d) Kwa makusudi huku akijua ni kosa atatoa taarifa za uongo kwa Halmashauri, au Atashindwa au kutoa taarifa zitakazohitajika na Halmashauri;

(e) Atashindwa kuweka kumbukumbu, vitabu, Hesabu au maelezo yoyote yatakayohitajika halmashauri; au

(f) Atamzuia Afisa Muidhiwa wakla kutekeleza majukumu yake.

Adhabu

9. Mtu yeyote atakayekwenda kinyume na masharti ya sharia Ndogo hizi na akipatikana na hatia atatozwa faini isiyozidi shilingi hamsini elfu (50,000/=) au kutumikia kifungo kisichozidi miezi kumi na mbili (12) jera au adhabu zote mbili kwa pamoja yaani faini na kifungo.

Kufifilisha kosa

10. Mkurugenzi anaweza kumtoza mtu yeyote faini isiyozidi sh. Elfu hamsini (50,000/=) iwapo mkosaji kwa hiari yake mwenyewe atakiri kosa kwa maandishi na kukubali kutekeleza wajibu wake na faini hiyo.

JEDWALI LA KWANZA
LIMEUNDWA CHINI YA KIFUNGU CHA 4 (I)

1. Kibali na ushuru wa madini ya Ujenzi.

Na	Uzito wa gari	Kiasi cha Ushuru
1	Maombi ya kibali cha kuchimba madini ya ujenzi	20,000/= kwa kila kibali
2	Madini ya ujenzi tani 1 hadi 3	10,000/= kwa kila safari
3	Madini ya ujenzi tani 3 hadi 7	15,000/= kwa kila safari
		1,000/=kila tani itakayoongezeka

2. Ada na kibali cha matangazo ya biashara

Na	Aina ya tangazo	Kiwango cha ushuru
1	Maombi ya kuweka mabango ya Biashara/kuchora	5,000/= kwa maombi
2	Matangazo yanayong'aa	4,000/= kwa futi za mraba kwa mwaka
3	Matangazo yanayong'aa	3,000/= kwa futi za mraba kwa mwaka
4	Tangazo kwenye kuta za nyumba	10,000/= kwa mwaka
5	Tangazo kwa kutumia kitambaa	5,000/= kwa mwezi/tukio
6	Matangazo ya vipaza sauti/magari na promosheni	20,000/= kwa kibali

3. Ada ya kukodi mali za Halmashauri

Na	Huduma	Kiwango
1	Kukodi ukumbi wa halmashauri kwa ajili ya mikutano/ vikao na sherehe	Kwa mujibu wa Mkataba
2	Kukodi viti	Kwa mujibu wa Mkataba
3	Kukodi gari , magari madogo	Kwa mujibu wa Mkataba
4	Magari makubwa	Kwa mujibu wa Mkataba
5	Mitambo(Trekta,Total station, vifaa vya GPS na kadhalika)	Kwa mujibu wa Mkataba
6	Vibanda vya biashara vya Halmashauri	Kwa mujibu wa Mkataba

4. Ada na vibali vya kuendesha shughuli za utamaduni burudani na michezo;

Na	Ada/ Ushuru	Kiwango
1	Kibali cha ngoma za jadi	5,000/= kwa siku
2	Kibali cha kupiga bendi za dansi, kuchezesha disco, michezo ya kubahatisha, sinema na sherehe	100,000/=kwa onyesho
3	Kibali cha kuchezesha sanaa za maonyesho	5,000/= kwa kibali
4	Kibali cha mechi za mashindano ya mipira na michezoPool table, football, Netball)	100,000/=kwa mashindano
5	Ada na usajili wa vitabu vya michezo, vikundi vya sanaa za utamaduni	5,000/= kwa mwaka

5. Ada ya huduma za machinjio, ukaguzi wa nyama na ushuru wa bucha

Na	Ada/Ushuru	Kiwango
1	Ada ya machinjio na Ukaguzi wa nyama kwa kila Ng'ombe atakayechinjwa	3,000/= kila mmoja
2	Ada ya Machinjio na Ukaguzi wa nyama kwa kila kondoo na mbuzi atakayechinjwa	1,000/= kila mmoja
3	Ada machinjio na ukaguzi wa nyama ya Nguruwe	2,000/= kila mmoja
4	Kuwamba na kukausha ngozi eneo la machinjio	
5	Ng'ombe	300/= kwa siku
6	Mbuzi, kondoo	100/= kwa siku
7	Ushuru wa Bucha la Ng'ombe, mbuzi, kondoo, nguruwe na samaki	500/=kwa siku

6. Ushuru wa gulio na soko

	Bidhaa / Huduma	Kiwango
1	Ushuru wa Meza/ kizimba Sokoni	200/= kwa siku
2	Ushuru wa mitumba	200/= kwa siku
3	Ushuru wa kizimba siku ya soko	200/= kwa siku
4	Pango la vibanda vya halmashauri	Kulingana na mkataba
5	Ushuru wa vibanda kuzunguka soko	500/=kwa siku
6	Ushuru wa vibanda kuzunguka vituo vya mabasi	500/=kwa siku

7. Ushuru wa mifugo na bidhaa za minada

	Aina ya mfugo	kiwango
1	Ng'ombe/ punda atakayeuzwa	Shilingi 5,000/=
2	Nguruwe	Shilingi 3,000/=
3	Mbuzi/kondoo atakayeuzwa	Shilingi 2,000/=
4	Kuku/Bata atakayeuzwa kwa tenga la watano watano	Shilingi 1,000/=
5	Ushuru wa ngozi mndani	
6	Ng'ombe/ punda	Shilingi 1,000/= kwa kila ngozi

7	Mbuzi /kondoo	Bei Shiliingi 500 kwa kila ngozi
8	Mama lishe/ Wauzaji wa vileo/nyama choma/na vyombo vya nyumbani na wafanyabiashara nyingine mnadani	Shilingi 1,500/= kwa siku
9	Ushuru wa asali na nta	5,000/= kwa kila lita 20
10	Vibali vya kusafirisha mizigo	
	Ngombe/punda	2,000/= kwa kila mnyama
	Mbuzi/kondoo/ Nguruwe	1,000/= kwa kila mnyama

8. Ada ya upimaji wa Ardhi na vibali vya Ujenzi

1	Mnara wa simu	500,000/=
2	Ghorofa moja	120,000/=
3	Nyumba za biashara	30,000/=
4	Nyumba ya makazi	25,000/=
5	Kituo cha mafuta	200,000/=
6	Majengo ya taasisi binafsi	200,000/=
7	Maghala na Bohari	120,000/=

NA	Ada ya mabadiliko (alieration) ya jingo lililopo	Kwa kila kibali
1	Nyumba ya kuishi na biashara	20,000/=
2	Nyumba ya biashara	60,000/=
3	Nyumba ya kuishi	10,000/=
4	Ghorofa	200,000/=
5	Kiwanda,bohari,ghala	60,000/=
6	Mabadiliko ya matumizi ya ardhi(makazi)	50,000
7	Mabadiliko ya matumizi ya ardhi(Biashara)	100,000/=

Ada za huduma ya Ardhi

1	Hati halisi ya Hati miliki(orginal R/O)	5,000/= kwa Nakala
2	Utafiti wa kitaalam (Official search)	5,000/=kwa kila huduma
3	Kubadili Hati Miliki (Transfer of R/O)	5,000/= kwa kila moja
4	Mchoro wa upimaji na ukaguzi wa ramani	10,000/=kwa kila mchoro
5	Kutambua eneo (plot identification)	10,000/= kwa kila plot
6	Kurudishia mawe yanaonesha mipaka (Beacon replacement)	5,000/= kwa kila jiwe

Ushuru wa stendi na maegesho ya Magari

1	Chombo cha usafiri	Ushuru wa maegesho
2	Teksi	1,000/=
3	Lori chini ya tani 7/ pick up/basi dogo	2,000/=
4	Lori zaidi ya Tani 7/basi kubwa	3,000/=
5	Magari mengine yasiyo ya biashara	500/= kwa siku
6	Ushuru wa kituo cha mabasi/stendi Mabasi yanayobeba abiria chini ya 25 Mabasi makubwa zaidi ya abiria 25	 1,000/= kwa siku 2,000/= kwa siku

Ada ya kuchangia uzoaji taka mijini (emerging towns)

Taasisi	Kiwango cha kuchangia kwa mwaka	Kiwango cha kuchangia kwa mwezi
Taasisi zote na mashirika	360,000/=	30,000/=
Viwanda vikubwa	600,000/=	50,000/=
Viwanda vya kuoka mikate(Bakery)	360,000/=	30,000/=
Hoteli ya kitalii	300,000/=	25,000/=
Migahawa	60,000/=	5,000/=
Useremala	50,000/=	4,200/=

Wauza mbao	60,000/=	5,000/=
Mashine ndogo za kusaga na kukoboa	30,000/=	2,500/=
Duka la jumla	60,000/=	5,000/=
Duka la rejareja	30,000/=	2,500/=
Ghala/godown	200,000/=	25,000/=
Viwanda vidogo vya kukamua mafuta	60,000/=	5,000/=
Bucha za samaki/nyama	30,000/=	25,000/=
Machinjio	300,000/=	25,000/=
Baa na mgahawa	60,000/=	5,000/=
Mini supermarket	60,000/=	5,000/=
Vitabu vya pombe Za kienyeji	30,000/=	2,500/=
Nyumba za kuishi	12,000/	1,000/=
Saluni za me na ke	25,000/=	2,500/=
Grocery (minibar)	30,000/=	2,500/=
Nyumba za kulala wageni	60,000/=	5,000/=
Vituo vya afya na zahanati	60,000/=	5,000/=
Vituo vya mafuta	150,000/=	13,000/=
Maduka ya vifaa vya ujenzi na	60,000/=	5,000/=
Maduka ya nguo naviatu	30,000/=	2,500/=
Maduka ya dawa(pharmacy)	60,000/=	4,200/=
Maduka ya dawa muhimu	30,000/=	2,000/=
Maduka ya mikate na vitafunwa	30,000/=	2,000/=
Maduka ya vyombo	30,000/=	2,000/=
Maduka ya kuuza magodoro na samani	30,000/=	2,000/=
Maduka ya kuuza spea za magari ,pikipiki na baiskeli	50,000/=	4,200/=
Maduka ya kuuza shajala na kurudufisha (photocopy)	50,000/=	4,200/=

Maduka ya kuuza vipodozi	30,000/=	2,000/=
Maduka ya kuuza simu/saa	25,000/=	2,000/=
Mama na baba lishe	24,000/=	2,000/=

9. Ushuru wa mazao

Zao	Kiwango cha ada /ushuru
Mahindi	2000/=@ gunia
Maharage	3000/=@ gunia
Mpunga	1500/=@gunia
Dagaa	2500/=@ gunia
Samaki	2000/=@ gunia
Vitunguu	2000/= @ gunia
Alizeti	2000/= @ gunia
Kabeji, machungwa,miwa,nanasi, ndizi, parachichi, embe	5000/= kwa tani moja, kabeji@ gunia 1000/=Ndizi@mkungu 500, machungwa @1000 tenga, parachichi, nanasi na embe@1000 kwa tenga
Viazi/mihogo	1000/=@gunia
Hoho	1000/= kwa tenga
Karanga za maganda	1500/=@gunia
Karanga zilizomenywa (kichere)	6000/=@ gunia
Njegere, mbaazi na jamii ya mikunde	2000/=@gunia
Nyanya	1000/=@ tenga
Mchele	5000/=@ gunia/kilo mia moja
Unga	3000/=@ gunia/ kilo mia moja
Ufuta	5000/=@ gunia kilo mia moja

10.Ada na Ushuru wa Huduma Nyingine

Ada ya kupima afya kwa wahudumu wa baa,Hotel na migahawa	5000/= kwa kila baada ya miezi mitatu
Adhabu ya papo kwa papo kwa mifugo inayokamatwa kwa kuzurura ovyo	
Ngombe /punda	20,000/= kwa kila mmoja
Nguruwe	20,000/= kwa kila mmoja
Mbuzi/kondoo	1000/= kwa kila mmoja
Ushuru wa kuhifadhi wanyama waliokamatwa kwa kuzurura ovyo	2000/= kwa kila siku
Ng'ombe/ punda	5000/= kwa kila mmoja kwa siku
Nguruwe	5000/= kwa kila mmoja kwa siku
Mbuzi/kondooo	3000/= kwa kila mmoja kwa siku

JEDWALI LA PILI

HATI YA KUKIRI NA KUFIFILISHA KOSA

(Chini ya kifungu cha 10)

Mimi …… nakiri mbele ya ……. Ambaye ni Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Nsimbo kwamba mnamo tarehe …….. ya mwezi …… Mwaka……..nilitenda kosa la kukiuka masharti ya kifungu cha ……cha sharia Ndogo za Halmashauri ya Wilaya ya Nsimbo (Ada na Ushuru) za Mwaka 2017.

Kwa Mamlaka aliyopewa Mkurugenzi Mtendaji Halmashauri ya Wilaya ya Nsimbo,Niko tayari kulipa kiasi cha Ada/ Ushuru ninaodaiwa pamoja na faini iliyoelekezwa na kifunghu cha 10 cha sharia ndogo hizi.

NATHIBITISHA KWAMBA MAELEZO HAPO JUU NI YA KWELI NA NIMEYATOA KWA HIARI YANGU KADRI YA UFAHAMU WANGU

Leo tarehe ……. Ya mwezi ……. Mwaka……..
Jina…….Saini ……

Mbele ya
Jina …….
Cheo……..
Saini……..

Nembo ya Halmashauri ya Wilaya ya Nsimbo imebandikwa kwenye Sheria Ndogo hizi Azimio lililopitishwa kwenye Mkutano wa Halmashauri uliofanyika tarehe ……Na kubandikwa mbele ya :-

MWAILWA SMITH PANGANI
Mkurugenzi Mtendaji
Halmashauri ya Wilaya ya Nsimbo

RAPHAEL A. KALINGA
Mwenyekiti
Halmashauri ya Wilaya ya Nsimbo

NAKUBALI,

Dodoma
9 Januari,2017

GEORGE B. SIMBACHAWENE (MB)
Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais- Tamisemi